LATRA

# VIGEZO NA MASHARTI YA MHUDUMU ALIYESAJILIWA NA LATRA KWA MUJIBU WA KANUNI ZA KUTHIBITISHA MADEREVA NA USAJILI WA WAHUDUMU WA MAGARI YA USAFIRI KIBIASHARA ZA MAMLAKA YA UDHIBITI USAFIRI ARDHINI ZA MWAKA 2020

Kwa mujibu wa kanuni ya 20(1) ya Kanuni za Kuthibitisha Madereva na Usajili wa Wahudumu wa Magari ya Usafiri Kibiashara za Mamlaka ya Udhibiti Usafiri Ardhini, Tangazo la Serikali Na. 81 la 2020 inamtaka mhudumu aliyesajiliwa kuhakikisha kuwa:-

a) Gari ya abiria haibebi mizigo hatarishi;
b) Gari ya abiria haibebi abiria zaidi ya idadi iliyoainishwa kwenye kadi ya gari;
c) Amevaa sare safi na nadhifu kama itakavyoamuliwa na Mamlaka;
d) Ana Kadi ya usajili iliyotolewa na LATRA;
e) Amewafahamisha abiria masuala yote ya usalama wa basi kabla ya kuondoka na wakati wa safari;
f) Vifaa vya kuhifadhi taka vipo ndani ya basi na vinatumiwa na abiria kuhifadhi taka;
g) Usafi wa ndani ya basi unazingatiwa wakati wote wa safari;
h) Amewapa abiria tiketi za kielektroniki katika mfumo wa karatasi au ujumbe wa simu ya mkononi;
i) Anatoa huduma bora kwa abiria;
j) Hatumii lugha chafu, kashfa au ya matusi kwa abiria;
k) Ameweka alama za utambulisho kwenye mizigo ya abiria na kuihifadhi sehemu salama;
l) Burudani inayotolewa ndani ya gari la usafiri wa umma wakati wote wa safari ipo katika sauti ya kiwango cha chini na inafuata maadili na utamaduni wa kitanzania;
m) Hakuna mtu yeyote anayefanya biashara, kuhubiri, kufanya shughuli za kisiasa au kutoa burudani ndani ya basi wakati wote wa safari;
n) Gari lina nakala tatu za taarifa za abiria kwa kila safari ambapo nakala moja itabaki;
    i. Kituo cha Polisi alipokaguliwa wakati wa kuanza safari;
    ii. Kwenye ofisi ya basi lilipoanzia safari; na
    iii. Ndani ya basi na ihuishwe wakati wote wa safari.